

FREDERICK EXAUD KILEO

YALIYOMO

Machache kuhusu kitabu cha Yuda. (1) 1
Machache kuhusu kitabu cha Yuda. (2). **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda (3) . **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda. (4) **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda. (5) **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda. (6) **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda (7) . **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda (8) . **Error! Bookmark not defined.**
1. Kuhusu njia ya Kaini. ..... **Error! Bookmark not defined.**
Uvumilivu wa Mungu ni nini? ..... **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda (9) . **Error! Bookmark not defined.**
2. Kuhusu kosa la Balaamu. ..... **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda. (10)**Error! Bookmark not defined.**
3. Kuhusu maasi ya Kora..... **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda (11). **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda (12) **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda (13) **Error! Bookmark not defined.**
Machache kuhusu kitabu cha Yuda (14).**Error! Bookmark not defined.**
KUHUSU HUDUMA. 10

Machache kuhusu kitabu cha Yuda. (1)

Yuda 1:1

[1] Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo, ndugu yake Yakobo, kwa hao walioitwa, waliopendwa katika Mungu Baba, na kuhifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo.

Yuda anaandika waraka huu kwa waamini, wale ambao wameitwa (walioitwa).

Waamini ni watu walioitwa kutoka giza na kuingia katika ufalme wa Nuru yaani ufalme wa mwana wa pendo lake ambako ni katika ukombozi yaani huo msamaha wa dhambi.

Wakolosai 1:13-14

[13] Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake;

[14] ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi;

Hivyo Yuda anaeleza jambo ambalo ni utambulisho wa mwamini.

Aliyeitwa, hii ina maana amehamishwa na kuwekwa katika ufalme mwingine tofauti na aliokuwa hapo kwanza kabla ya kuamini au kuitwa.

Pili, Yuda anasema wito wa Mungu ni hilo pendo katika Mungu Baba. Pendo la Mungu ni huo ukombozi katika Kristo Yesu yaani msamaha wa dhambi.

Tatu, Yuda anasema hao walioitwa ambao ndio hao ambao wamependwa katika Mungu wanahifadhiwa kwaajili ya Yesu Kristo.

1 Petro 1:5

[5] Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho.

Hayo mambo matatu ambayo Yuda anaeleza katika mstari huu wa kwanza ni ya muhimu na kuzingatiwa maana ni utambulisho wa mwamini ndani ya Kristo Yesu.

1. **Ameitwa**
2. **Amependwa katika Mungu Baba**
3. **Ana(me)hifadhiwa kwaajili ya Yesu Kristo.**

Yuda ameeleza mambo hayo si kwasababu ya jina tu la mwamini hali kueleza uhalisia mwamini na kile ambacho ni halisi kwa mwamini.

Mwamini anaweza asijue mambo hayo kwasababu ya kukosa bidii katika kujifunza ama kusikia, ama kwa kukosa fundisho sahihi katika kanisa la mahali, Lakini inabaki kweli kwamba mwamini ameitwa, amependwa katika Mungu Baba na hata kuhifadhiwa kwaajili ya Yesu Kristo.

Yuda 1:2

[2] Mwongezewe rehema na amani na upendano.

Yuda anaendelea kuwajulisha waamini hawa (katika maombi) ili waongezeke katika rehema na amani na upendano.

Hapa Yuda hakua anasema waamini wana upungufu wa hayo mambo wala hakurejea kuwa mambo hayo ni katika upungufu kwao.

Kwanza kabisa, Mwamini ni mtu ambaye ana rehema zote za Mungu, ana amani yote ya Mungu na pia ana upendo wote wa Mungu.

1. **Mwamini amepata rehema**

1 Petro 2:9-10

[9] Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu;

[10] ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema.

Mwamini hana upungufu wa rehema, ni mwenye rehema tayari.

2. **Mwamini ana amani ya Mungu.**

Yohana 14:27

[27] Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga.

Mwamini ana amani na Mungu kwasababu amehesabiwa haki kwa imani .

Warumi 5:1

[1] Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,

Neno "mwe na amani" ni tafsiri mbovu katika lugha ya Kiswahili. Kwenye kiingereza na lugha ya Kigiriki inaonesha amani sio kitu ambacho mwamini anatafuta kuwa nacho, bali imeonesha mwamini anamiliki amani, ana amani na Mungu kwasababu amehesabiwa hali kwa imani.

"Therefore being justified by faith, we have peace with God through our Lord Jesus Christ:" (Romans 5: 1)

3. Mwamini ana upendo wa Mungu.

Warumi 5:5

[5] na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.

Kwahiyo maombi ya Yuda si maombi ya kupokea, bali ni maombi ya ukuaji wa kiroho.

Ni maombi kwamba mwamini ajue na kisha kuishi katika uhalisia wa kile anachokijua kutokana na kazi ya ukombozi alioufanya Kristo Yesu.

Hivyo kuongezeka katika rehema, amani na upendano ni ukuaji wa kiroho, katika ufahamu/nia (nafsi) apate kujua mapenzi ya Mungu na kuenenda kwayo.

Paulo na mitume wamefundisha hilo kuhusu ukuaji wa kiroho na mwenendo wa mwamini kati ya watakatifu.

Hivyo kuongezewa rehema amani na upendano ni lugha ya kumsisistiza ama kumuombea mwamini apate kujua kweli (epignosis) na kutembea katika ujuzi wa hiyo kweli kati yake na waamini wengine.

Petro anasema:

2 Petro 3:18

[18] Lakini, **kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo.** Utukufu una yeye sasa na hata milele.

Neema haikui, mwamini anakua katika kweli kwa kumjua sana mwana wa Mungu. Hivyo neema kwa mwamini inasemwa kuwa imekua kwa mwamini kuongezeka katika maarifa na mwenendo katika hayo maarifa kati yake na waamini wengine.

Yohana naye amefundisha kuhusu ukuaji wa kiroho.

3 Yohana 1:2-4

[2] Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya yako, kama vile roho yako ifanikiwavyo.

[3] Maana nalifurahi mno walipokuja ndugu na kuishuhudia kweli yako, kama uendavyo katika kweli.

[4] Sina furaha iliyo kuu kuliko hii, kusikia ya kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli.

Mwenendo katika Kweli, ushuhuda katika kweli.

2 Yohana 1:2-5

[2] kwa ajili ya hiyo kweli ikaayo ndani yetu, nayo itakuwa pamoja nasi hata milele.

[3] Neema, na rehema, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Yesu Kristo Mwana wa Baba, zitakuwa pamoja nasi katika kweli na upendo.

[4] Nalifurahi mno kwa kuwa nimewaona baadhi ya watoto wako wanaenenda katika kweli, kama vile tulivyopokea amri kwa Baba.

[5] Na sasa mama, nakuomba, si kwamba nakuandikia amri mpya, bali ile tuliyokuwa nayo tangu mwanzo, kwamba tupendane.

Msisitizo ni katika kujua kuwa tuna pendo, hivyo tuenende katika huo upendano.

Paulo amesisitiza hilo mathalani katika nyaraka zake zote.

Waefeso 1:17-20

[17] Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye;

[18] macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo;

[19] na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake;

[20] aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho;

Ni katika kujua mambo mema yote yaliyopo kwetu ndani ya Kristo Yesu.

Filemoni 1:6

[6] ili kwamba ushirika wa imani yako ufanye kazi yake, katika ujuzi wa kila kitu chema kilicho kwetu, katika Kristo.

Wafilipi 1:9-11

[9] Na hii ndiyo dua yangu, kwamba pendo lenu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote;

[10] mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo;

[11] hali mmejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.

Wakolosai 1:9-12

[9] Kwa sababu hiyo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu, ili mjazwe maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni;

[10] mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa; mkizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu;

[11] mkiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wake, mpate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha;

[12] mkimshukuru Baba, aliyewastahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru.

Turudi kwa Yuda.

Yuda anaendelea kuonesha msisitizo wa namna rehema na amani na upendano unaongezwa kwa hao waamini.

Yuda 1:3

[3] Wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu.

Ni katika kujua hizo habari za wokovu ambao wamekabidhiwa mara moja kwa imani, hivyo wanaongezeka katika kuishindania yaani kujua na kudumu katika mwenendo wa hiyo kweli.

Kwahiyo mwamini anaishindania imani aliyokabidhiwa mara moja kwa kudumu katika fundisho la kweli, yaani fundisho la wokovu kwa imani katika Kristo Yesu.

Msisitizo huo ni kwasababu kuna watu wanajiingiza kwa siri na mafundisho ya uongo ili kuwaharibu hao waamini.

Yuda 1:4

[4] Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, makafiri, wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, nao humkana yeye aliye peke yake Mola, na Bwana wetu Yesu Kristo.

Yuda anaeleza neema ya Mungu ni katika Kristo Yesu ila wapo wapotoshao na kuibadili neema hii na kuifanya ufisadi, watu hao ni makafiri. Watu wasio na Mungu, watu wasiomjua Mungu. Watu walio tayari kwaajili ya hukumu ya adhabu.

Paulo amefundisha kuwa neema ya Mungu ndio Injili, hivyo wasiofundisha neema ya Mungu ni watu walioanguka kutoka katika hali ya neema, ni watu wataabishaji.

Wagalatia 1:6-7

[6] Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine.

[7] Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo.

Hivyo watu wasiomhubiri Kristo, wameanguka kutoka kwenye neema ya Mungu. Ni wataabishaji, ni watu walioandikiwa hukumu tangu zamani.

Itaendelea...

KUHUSU HUDUMA.

Kazi yetu ni kufundisha na kuhubiri NENO kote ulimwenguni, katika kila taifa, kwa kila lugha na kabila, katika kila mkoa, utamaduni, bara na nafasi ya Dunia.

Kwa hivyo, tumejitolea kufundisha, kufundisha na kuhamasisha waumini katika Ukweli, Ukomavu na Huduma katika Kristo Yesu - NENO.

Hii tunafanya na msisitizo mkubwa juu ya hali halisi ya uumbaji mpya ndani ya Kristo.

Tunajitahidi kufundisha na kuhubiri injili hii pamoja na ufahamu wake wa Kristo wa ishara maalum na maajabu - Miujiza.

Tuna Darasa la Bibilia (SBC) ambalo ni huduma yetu ya kanisa ambapo mara kwa mara tunamkuza muumini kupokea na kuhudumu misheni hii, kwa kuwasiliana mara kwa mara juu ya maono yetu.

Tutaiona Dunia yote ikiwa imefunikwa na ujuzi wa utukufu wa Mungu, kama vile maji yanavyofunika bahari (Hab 2:14).

Yesu Kristo ni Bwana !

Tunashinda!

Saints Bible Church (SBC)

Telegram: https://t.me/Soundbibleclass

Facebook: Fekileo Ministries International

At The University of Dodoma: contact us through 0719267857/0693372819